# JARIDA LA

## CHUO CHA BAHARI DAR ES SALAAM(DMI)

MATUKIO YA DMI

TOLEO NA:1 JULAI 2023 - JUNE 2024

ISSN 3057 - 3025

**DMI-Kituo cha Ubora cha Elimu na Mafunzo ya Bahari Afrika Mashariki**





## *SAFARI YA DMI KUANZIA MWAKA 1978 NA MAFANIKIO YAKE KWA KIPINDI CHA MIAKA 60 YA MUUNGANO*







# Neno kutoka kwa Mkuu wa Chuo



Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) kimeanzishwa kwa sheria ya Bunge namba 2 ya mwaka 1991. Ni Taasisi ya Elimu ya juu iliyopo chini ya usimamizi wa Wizara ya Uchukuzi. Kabla ya kuanzishwa kwa sheria ya Bunge Chuo cha Bahari Dar es Salaam kilikua ni kitengo cha mafunzo kilichokuwa kikitoa elimu na mafunzo ya Ubaharia pekee kilichojulikana kama DMTU

Sheria ya mwaka 1991 ilikipa Chuo majukumu yake ambayo kinatekeleza hadi sasa yaani, kutoa elimu na mafunzo yanayohusu Bahari zikiwemo kozi za umahiri za ubaharia (Certificate of Competence), Kufanya tafiti na kutoa machapisho, kutoa ushauri elekezi kwa Taasisi za Umma na Binafsi

Kozi za Ubaharia zinazotolewa na DMI zinaithibati ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) na kufanyiwa kaguzi za kimataifa na Shirika la Bahari Duniani (IMO) na Msajili wa Kimataifa Det Norske Veritas (DNV) kwa ubora wa viwango vya ISO 9001:2015.

Chuo kina jumla ya program (NTA Levels) arobaini na moja (41) zenye ithibati ya NACTVET zikiwemo za Usanifu wa vyombo vinavyofanya shughuli za kwenye maji, usafirishaji wa njia ya maji, uhandisi wa mafuta na gesi baharini, Biashara za kimataifa na sheria za baharini.Kozi fupi 45 na kozi za Umahiri 11.

Kozi za ufundi (NTA) zinasimamiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) zipo kuanzia ngazi za Astashahada (cheti) hadi Shahada za uzamili. Wahitimu wanaomaliza kozi za Chuo cha Bahari Dar es Salaam wanafanya kazi ndani na nje ya nchi hususani wale wa kozi za ubaharia.

Wahitimu wa kozi zetu wanaweza kufanya kazi katika maeneo mengi kama vile mashirika ya meli, kampuni za usafirishaji, taasisi za mafunzo ya baharini, bandari, mamlaka za baharini, mashirika ya usafirishaji, mashirika ya uokozi, kampuni za utafiti wa baharini, kampuni za bima za usafirishaji, kampuni za uzalishaji wa viwandani, kampuni za madini na Utafutaji wa mafuta na gesi.

Aidha, katika kuendana na ongezeko la uhitaji wa soko katika sekta ya bahari, Chuo kimeendelea kuongeza wafanyakazi wenye uzoefu na weledi katika kutoa mafunzo, utafiti na ushauri wa kitaalamu wa hali ya juu.

Kwa niaba ya Bodi ya Chuo, wafanyakazi na jumuiya yote ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), ninakukaribisha kwa moyo mkunjufu kujiunga na DMI ili kutimiza ndoto zako.
Asante.

**Dkt.Tumaini S.Gurumo**
**Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)**

# Dhima

Kuwa taasisi bora katika mafunzo, utafiti na ushauri katika taaluma za baharini na zinazohusiana.

# Dira

Kutoa mafunzo ya hali ya juu yanayo endeshwa na mahitaji, utafiti na huduma za ushauri katika taaluma za baharini na taaluma zinazo husiana katika ukanda wa kusini mwa jangwa la Sahara na kwingineko.

# TAHARIRI




Karibu mpenzi msomaji wa Jarida Toleo la kwanza la Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) .Jarida hili litakuwa likitolewa mara mbili kila mwaka yaani Januari -Juni na Julai- Desemba. Jarida hili linalenga kuhabarisha Umma juu ya matukio yaliyofanyika Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), kuelimisha wananchi juu ya fursa zitokanazo na Sekta ya Bahari ikiwemo Uchumi wa Buluu na kutangaza kozi zinazotolewa na Chuo ili kuruhusu wananchi kujiunga. Jarida hili pia limekusudiwa kuwafikia wananchi wa maeneo mbalimbali kupitia njia ya mtandao kupitia tovuti rasmi ya Taasisi ambayo ni www.dmi.ac.tz. Vilevile, nakala za jarida hili zitasambazwa ili kuwa nyenzo muhimu na daraja la kuunganisha wananchi na DMI, huku likisaidia kufikia lengo la kuhakikisha Chuo kinaendelea kutoa mafunzo bora yanayozingatia mahitaji ya sasa, utafiti, na huduma za ushauri katika taaluma za baharini na taaluma zinazohusiana, hususan katika Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara na maeneo mengineyo.

Asante na tunawatakia usomaji mwema.


**BODI YA WAHARIRI**

MWENYEKITI

Bw.Mansour R. Likamba

MAKAMU MWENYEKITI

Dkt.Wilfred J. Kileo

**WAHARIRI**

Bw.Jonnes J. Lugoye

Bw. Mashambo K. Washington

**MSANIFU**

Bi.Alda P. Sadango



CHUO CHA BAHARI DAR ES SALAAM
S.LP 6727
Posta, Sokoine Drive,Dar es Salaam.
Barua pepe :info@dmi.ac.tz
Tovuti : www.dmi.ac.tz
Nukushi: +255222133645
Simu: 0738260013/0738260049
Msanifu: 0658438943

**MITANDAO YA KIJAMII**

: dmi_tanzania
: dmi_tanzania
: dmi_tanzania
: DMI TV


# YALIYOMO


**1. Safari ya DMI kuanzia mwaka 1978 (UK 4-9)**

**2. Ushirikiano wa DMI na Taasisi za Ndani na Nje ya Nchi (UK 10-12)**

**3. DMI Yapongezwa Kuzalisha Wataalamu Wanoendana na Teknolojia(UK 13)**

**4. Baraza la 6 la Wafanyakazi wa DMI Lazinduliwa (UK 14)**

**5. Uongozi wa IMO Watembelea DMI kuona Maendeleo ya Utendaji kazi (UK 16)**

**6. DMI,TASAC na Mamlaka ya Bahari ya Bahamas Kushirikiana kukuza Sekta ya Usafiri wa Majini(UK 17)**

**7. Wahitimu 1326 Watunukiwa Vyeti kwenye Mahafali ya 19 ya Chuo cha Bahari (UK 18)**

**8. Serikali Yaombwa Kuipatia DMI Meli ya Mafunzo kwa Vitendo (UK 19 )**

# Safari ya Chuo cha DMI Kuanzia Mwaka 1978




*Naibu Waziri wa UChukuzi Mhe.David Kihenzile akihudhurisha wahitimu kwenye mahafali ya 19 yaliyofanyika Novemba 30, 2023 katika viwanja vya DMI*

Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), kilianzishwa mwaka 1978 baada ya kuvunjika Umoja wa Nchi za Afrika Mashariki (EAC).

Akizungumzia historia kwa ujumla ya DMI, Mkuu wa Chuo, Dkt. Tumaini Gurumo, alisema wakati wa Umoja wa Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki, shughuli mbalimbali, zilifanywa kwa ushirikiano kati nchi wanachama.

Alisema baada ya kuvunjika umoja huo, Tanzania ilibahatika kupewa meli, lakini ikagundulika hakukuwa na Watanzania ambao wangeweza kuziendesha.

"Baada ya kugawiwa meli, ilibainika kwamba, hakukuwa na Watanzania walioweza kupewa jukumu la kuziendesha meli hizo, kwani hatukuwa na manahodha,» alisema Dkt. Tumaini.

Alisema baadae, ukaanzishwa utaratibu wa Tanzania kuwa na chuo cha bahari, lengo likiwa kuwafundisha Watanzania,

**"Baada ya kubaki na meli, ilibainika kwamba, hakuna Watanzania wanaoweza kupewa kuendesha meli hizo, kwani hatukuwa na manahodha wala wahandisi," alisema Dk. Tumaini.**

kwa sababu kusoma taaluma hiyo nje ya nchi ni gharama

Alieleza kuwa, kutokana na umuhimu huo, chuo hicho cha bahari, kilianza kama kitengo, kilichokuwa chini ya Wizara ya Uchukuzi, kilianza kufundisha mabaharia kwa ngazi za chini.

## FANI YA UBAHARIA

Kwa mujibu wa Dkt. Tumaini, ubaharia ni fani kama zilivyo nyingine, ina ngazi zake kama taaluma nyingine ambapo mhusika huanzia chini na kupanda hatua kwa hatua.

Alifafanua zaidi kuwa, mabaharia hao, wanatofautiana kulingana na elimu walizopata na ukubwa wa chombo ambacho atakachofanyia kazi.

Alieleza kuwa, chuo kilipoanzishwa, walikuwa wakitoa mafunzo kwa mabaharia wa ngazi saidizi hadi ngazi ya afisa daraja la tatu.


Kwa sasa Chuo kinatoa mafunzo hadi ngazi ya daraja la kwanza kwa manahodha (Master Mariners) na wahandisi wa meli (Marine Chief Engineers).

**MWAKA 2003**

Kwa mujibu wa Dkt. Tumaini, mwaka 2003, ubora wa mafunzo yanayotolewa na Chuo ulifanikisha Nchi ya Tanzania kuingizwa katika orodha ya 'White List' hivyo, kuwezesha mabaharia wanaohitimu hapa nchini kutambulika kimataifa na kupata kazi nchi yoyote duniani

Alisema kuwa, hatua ya uingiaji katika 'white list' ni mchakato kwani, zipo baadhi ya nchi, hazijafikia hivyo.

"Kwetu ni mafanikio makubwa kwa sababu, kuna nchi jirani hadi sasa hazijafanikiwa kuingia katika 'White List,' lakini Tanzania kama nchi tumefanikiwa kuwepo tangu mwaka 2003.



# Safari ya Chuo cha DMI Kuanzia Mwaka 1978

Aidha, Dkt.Tumaini, alisema kuwa, elimu ya ubaharia, unahitaji wanafunzi kufanya vitendo baada ya nadharia ya darasani, hivyo vifaa vinahitaji zaidi.

Hata hivyo, kabla ya kuingia katika 'White List', ilifanyika juhudi kubwa ya kuwa na vifaa vya kisasa vya kufundishia kwa sababu elimu ya ubaharia imejikita katika vitendo zaidi kuliko nadharia.


"Tunapofundisha darasani, kuna wakati inatulazimu kwenda kufanya mafunzo kwa vitendo, hatua hii inahitaji zaidi kuwa na mitambo ya 'Simulators, ambayo ina kila kitu kinachoweza kupatikana

## MITAMBO NA VIFAA VYA KUFUNDISHIA


katika meli.' alisema Dkt. Tumaini

Aliongeza kuwa hata ule upande wa chumba cha nahodha ambacho anakitumia, nako kuna kila kitu," alisisitiza.

Alisema kuwa na mitambo hiyo pamoja na karakana ya uhandisi ni miongoni mwa vigezo na sifa zilizofanya chuo kuendelea kuboresha utoaji wa elimu na mafunzo kwa vitendo katika tasnia ya bahari.



*Mwanafunzi wa DMI akiwa kwenye mafunzo ya Vitendo*



*Chumba cha mtambo wa kufundishia wanafunzi wanaosoma masomo ya Uhandisi wa meli unaojulikana kama Engine Simulator*

# Idadi ya wanaosoma kozi za ubaharia yapaa kwa kasi

Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), kilianza kutoa mafunzo ya ubaharia na uhandisi kikiwa na wanafunzi 12.

Kadri miaka iliyoongezeka idadi na mwitikio wa wanafunzi kutaka kusomea taaluma hizo, uliendelea kuongezeka.

Katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa, maarufu kama Sabasaba Mwaka 2023 Yaliyofanyika Viwanja vya Mwl. Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam wananchi wengi hasa vijana, walijitokeza katika banda la DMI, wakitaka kufahamu mambo mbalimbali na utaratibu wa kujiunga.

Mkuu wa Kitengo cha Udahili wa Chuo , Bw. Bernard Mgendwa, alisema kumekuwa na mwitikio mkubwa kwa vijana kujiunga na fani mbalimbali ikiwemo ya ubaharia.

Bw. Mgendwa alisema kuwa, Chuo, kimeshiriki maonesho hayo kueleza shughuli za kitaaluma, fursa zinazotokana na Uchumi wa Buluu kupitia Bahari, Mito na Maziwa.

Alieleza kuwa, DMI imekuwa ikitoa kozi na programu mbalimbali za bahari kwa watu binafsi na nchi mbalimbali za jirani, zikiwemo, Kenya, Uganda, Comoro, Rwanda, Burundi, Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Namibia.

Aidha, DMI inatambulika kwa programu zake za mafunzo ya ubora wa hali ya juu katika taaluma ya bahari kwa kufuata viwango vya kimataifa.

# Safari ya Chuo cha DMI Kuanzia Mwaka 1978



*Wanafunzi wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam wakiwa wanajisomea katika Maktaba ya Chuo hicho.*

Mkuu wa Chuo Dkt. Tumaini Gurumo, alisema, kumekuwa na mwamko mkubwa wa Watanzania kutaka kusoma taaluma ya bahari, ikilinganishwa na ilivyokuwa wakati DMI inaanzishwa mwaka 1978.

Dk. Tumaini, alisema kwa mwaka 2024, wanafunzi wamefikia idadi ya 5,177 wa kozi ndefu na 6,000 wa kozi fupi huku idadi ikiendelea kuongezeka kila mwaka.

Akieleza kasi ya ongezeko hilo, Dkt. Tumaini alisema mwaka wa masomo wa 2022/2023 , wanafunzi walikuwa 3,505 huku mwaka 2021/2022, walikuwa 2,299, na mwaka 2020/2021 walikuwa 1,590 hali inayoonesha chuo kupiga hatua kubwa.

## MWAMKO ZAIDI ZANZIBAR

Dkt. Tumaini, alisema kuwa, licha ya kuwepo kasi hiyo ya ongezeko la idadi ya wanafunzi, vijana kutoka visiwani Zanzibar, wameonekana kuwa na mwamko mkubwa zaidi ikilinganish wa na wanaotoka Tanzania Bara.

““Wanafunzi wanaotoka Zanzibar ndiyo wanaojiunga kwa wingi chuoni ukilinganisha na Bara.

“Sababu ya kuwa na mwamko mkubwa, inatokana na shughuli zao nyingi kutegemea bahari.

“Zanzibar ni kisiwa, hivyo wakazi wake wengi kazi zao nyingi zinatokana na uvuvi.

“Hivyo, wamekuwa na shauku zaidi ya kutaka kusoma masuala ya bahari ukilinganisha vijana wa Tanzania bara,” alifafanua Dk. Tumaini.

## HAMASA TANZANIA BARA

Alisema kuwa, zimekuwa zikifanyika jitihada za makusudi za kuhakikisha Watanzania au vijana kutoka Tanzania Bara, wanajiunga na Chuo cha Bahari.

Dk.Tumainialisema inawezekana hapo awali vijana hawakuwa wakiziona fursa katika bahari, lakini mwitikio unaendelea kuimarika mwaka hadi mwaka.

## MAJUKUMU MENGINE YA DMI

Kwa mujibu wa Dkt. Tumaini, Sheria Namba 22 ya mwaka 1991 iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge, ilitoa majukumu kwa DMI kama Taasisi ya Elimu ya Juu na kupewa kazi muhimu, mojawapo ikiwa ni kutoa elimu na mafunzo.

Pamoja na kuendelea na jukumu la kufundisha, DMI pia inahusika ‘kupika’ rasilimali watu katika maeneo yote ya shughuli za maji.



*Wanafunzi wa DMI wakiwa kwenye mafunzo kwa vitendo ya Personal Survival Techniques.*

# Safari ya Chuo cha DMI Kuanzia Mwaka 1978



*Wahitimu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) wakiwa kwenye Mahafali ya 19 November yaliyofanyika November 30*

## UHUSIANO WA TASAC NA DMI

Dkt. Tumaini, alisema kwa sababu Tanzania ilisaini mkataba wa kimataifa unaoongoza au kusimamia mafunzo ya mabaharia, ilipaswa kuwa na mamlaka inayojitegemea .

Hivyo Serikali ilianzisha Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), ambalo pamoja na mambo mengine, ndiyo msimamizi mkuu wa shughuli za bahari na maziwa nchini.

"TASAC inahusika kukagua mitaala ya kozi za ubaharia zinazofundishwa na chuo.

"TASAC Lazima ipitie mitaala yetu kisha kuridhia kutumika baada kufuata vigezo vyote vya kimataifa vinavyohitajika," alisema Mkuu wa Chuo.

Aidha, alisema kwamba, hata mitihani inapoandaliwa, kabla ya kufanyika, TASAC huwa na jukumu la kuikagua kuhakikisha kwamba imekidhi vigezo.

Lengo la TASAC ni kuhakikisha ubora wenye viwango vya kimataifa, vinazingatiwa.

"Chuo hukaguliwa na TASAC ili kujiridhisha kama kuna rasilimali watu wa kutosha na vifaa vya kutosha, kwa mujibu wa sheria ya kimataifa inavyoelekeza.

"Pia, alieleza kuwa 'International Maritime Organization' (IMO), wanaosimamia sheria za ubaharia, huja nchini kila baada ya miaka mitano kufanya ukaguzi na kutoa ushauri kuhusu elimu na mafunzo."

## USHIRIKIANO NA TAASISI NA VYUO VYA NJE

DMI, imekuwa na uhusiano na Taasisi pamoja na Vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi, hatua ambayo imekinufaisha Chuo.

Baadhi ya nchi alizozitaja kuwa na ushirikino ni pamoja na China, Norway, Italia, Korea Kusini na Ghana.

Alifafanua miongoni mwa manufaa wanayopata kupitia ushirikiano huo, mojawapo ni wanafunzi kupata nafasi katika meli za kufanyia mafunzo kwa vitendo.

"Chuo hakina meli za kufanyia mafunzo kwa vitendo, hivyo kutokana na uhusiano na ushirikiano uliopo, wanafunzi wetu wanapata nafasi katika meli za mataifa hayo". alisema Dkt. Tumaini

**DMI YAIPONGEZA SERIKALI**

Dkt. Tumaini, aliishukuru Serikali kwa kutambua uhitaji wa rasilimali watu ambao wamekuwa wakiongezwa kila inapohitajika.

Alisema wapo walimu wanaofundisha kwa mkataba, ingawa ni wachache, lakini wana weledi mkubwa unaowatosha kutoa taaluma stahiki kwa ngazi zote.

Pia, DMI inatoa ushauri kwa serikali na kampuni binafsi kuhusu masuala ya majini. Hii ni kutokana na ukweli kwamba baadhi ya wataalam wanaoshiriki katika ujenzi na ukaguzi wa meli wanatoka Chuo cha Bahari.

**MKUU WA CHUO MZAWA**

Dkt. Tumaini, alisema mwaka 1990, DMI ilipata Mkuu wa Chuo wa kwanza mzawa, baada ya kuongozwa na raia wa Norway tangu kuanzishwa kwake kwani kabla ya kipindi hicho, Watanzania hawakuwa na uwezo huo.

Alieleza kuwa, katika kuzingatia masuala ya jinsia, mwaka 2023, aliteuliwa rasmi kuwa Mkuu wa Chuo wa kwanza, mwanamke.

**KUHUSU DK. TUMAINI:**

Dk. Tumaini, ambaye ni Mkuu wa chuo wa kwanza mwanamke, ni mhadhiri mwandamizi na amefundisha chuoni hapa, tangu mwaka 2005.

# Safari ya Chuo cha DMI Kuanzia Mwaka 1978




*Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam Dkt. Tumaini Gurumo akitazama moja ya dokumenti katika ofisi yake.*

Awali, alikaimu nafasi ya Mkuu wa Chuo kwa miaka miwili mfululizo kabla ya kuteuliwa rasmi kuongoza DMI.

Dkt. Tumaini ana uzoefu mkubwa katika masuala ya bahari.Pia, ana fundisha kozi mbalimbali zikiwemo za sheria za bahari, masuala ya bima na ubebaji mizigo baharini.

Amewasimamia wanafunzi wengi huku naye akishiriki katika kuandaa kanuni, sera na mengine yanayohusu bahari.

Dkt. Tumaini ndiye mtunzi wa kitabu alichokipa jina; "UCHUMI WA BLUU: Fursa na Chachu ya Maendeleo."

### MIKAKATI MINGINE

Dkt. Tumaini, alisema kwamba, licha ya kupata eneo la kujenga tawi la chuo Pemba, kuna mkakati wa kuongeza wigo katika Mkoa wa Lindi ambako elimu inahitajika kutokana na uwepo wa mafuta na gesi ambavyo vinachimbwa baharini.

"Mipango ya miaka ijayo ni kuangalia eneo la Lindi ambako limepatikana eneo la ujenzi wa tawi la chuo,, maeneo mengine ni Nyamagana- Mwanza , Busega -Simiyu na Mkurunga-Pwani " alisema Dkt. Tumaini.

# Jinsi DMI ilivyobeba Jukumu la Kuutangaza Uchumi wa Buluu

TANGU kuingia madarakani Mhe.Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Nane imekuwa ikiweka mkazo mkubwa katika kukuza uchumi kupitia rasilimali za bahari.

Katika kuhakikisha inatoa kipaumbele hicho, Rais Dkt. Mwinyi, aliamua kuunda Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ambayo ni mahususi kushughulikia masuala yote ya rasilimali za bahari.

Wakati akizungumza na mabalozi wateule, Ikulu ya Zanzibar, Oktoba 04, 2023 ambao walikwenda kujitambulisha kwake, Rais Dk. Hussein, alisema Zanzibar bado ina mahitaji makubwa ya uwekezaji katika sekta ya uchumi wa Buluu kupitia utalii na ufugaji wa vifaranga vya samaki.

Katika mazungumzo yake, aliwataka mabalozi kuzichangamkia fursa za uwekezaji katika nchi wanazoziwakilisha na kuwavutia wawekezaji kuja Zanzibar, lengo likiwa kuimarisha uchumi wa nchi unaochangia asilimia 30 ya pato la taifa.

Pamoja na mabalozi kupewa maelekezo hayo, Chuo cha Bahari Dar es Salaam, nacho kimebeba jukumu la kuendelea kuwa kitovu cha ubobezi na kuendeleza dhana ya uchumi wa buluu.

Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam Dkt. Tumaini Gurumo, alitoa pongezi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa namna ilivyotoa kipaumbele katika uchumi wa buluu.

Dkt. Tumaini, alieleza namna DMI ilivyoamua kubeba jukumu la kuutangaza uchumi wa buluu ambao una fursa nyingi zilizopo baharini ambazo baadhi ya nchi zingine hazina baraka hiyo.

Pongezi kwa Serikali za Zanzibar kwa kuona fursa zilizopo baharini, lengo ni kujipatia faida za kiuchumi.Tuna bahari ambayo samaki waliopo wanauzwa nje ya nchi.

"Faida ni nyingi ambazo sisi DMI,tunapaswa kuzieleza kwa sababu ni jukumu letu kufanya hivyo,» alisema Dkt. Tumaini.

Dkt. Tumaini alisema kwa sababu, DMI ina wajibu wa kutoa elimu, ushauri, mafunzo na mambo mengine katika masuala

# Jinsi DMI ilivyobeba Jukumu la Kuutangaza Uchumi wa Buluu

yanayohusu bahari, wamekuwa wakifanya makongamano kila mwaka kuhusu uchumi wa buluu.

Alieleza kuwa, mwaka 2024, DMI itafanya Kongamano la Kimataifa, ambalo litawahusisha watalaamu kutoka maeneo mbalimbali barani Afrika na nchi zingine kwa lengo la kubadilishana uzoefu.

“Tutapata wasemaji waliobobea katika eneo la uchumi wa buluu, kama nchi ya Mauritius ilivyofanikiwa, tunataka kujifunza kutoka kwao.

“Wanapiga hesabu jinsi walivyofanikiwa kutokana na matumizi mazuri ya maji,» alisema Dk. Tumaini.

Alifafanua zaidi kuwa, huo ni mkakati wa Bara la Afrika kuhakikisha bara linanufaika kutokana na rasilimali zake zilizopo katika bahari.

“Niliwahi kuandika kitabu kinachoelezea fursa za bahari, tena nilitumia lugha ya kiswahili Watanzania wengi waweze kusoma kilichomo. Miongoni mwa kazi zetu kama DMI ni kufanya utafiti na utoaji elimu kupitia maandiko kama hayo,” alieleza Dkt. Tumaini.

“Niliwahi kuandika kitabu kinachoelezea fursa za bahari, tena nilitumia lugha ya kiswahili Watanzania wengi waweze kusoma kilichomo. Miongoni mwa kazi zetu kama DMI ni kufanya utafiti na utoaji elimu kupitia maandiko kama hayo Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)”Dk. Tumaini Gurumo




*Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam akitoa taarifa ya kongamano la 3 la uchumi wa buluu kwa waandishi wa habari Juni 27,2024*

Juni 27, 2024 wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Kongamano la Tatu la Kimataifa la Uchumi wa Buluu, Dkt. Tumaini alitoa wito kwa Watanzania kushirikiana na DMI katika kufanikisha shughuli hiyo itakayofanyika Julai 4 na 5, 2024 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Dkt. Tumaini alisema kongamano hilo, linafanywa na DMI kwa kushirikiana na Chuo cha Regional Maritime University (RMU), kilichopo nchini Ghana, kwa lengo la kukutanisha wadau wa uchumi wa buluu ili kujadiliana na kubadilishana uzoefu katika kukuza dhana ya uchumi wa buluu barani Afrika.

“Kongamano hili linaandaliwa na DMI kwa sababu ndiyo Chuo pekee katika nchi kilichopewa dhamana ya kufundisha masuala yanayohusu bahari kwa upana wake.



**MKAKATI MWINGINE**

Dkt. Tumaini alisema DMI, inakusudia kupita katika maeneo kunakofanywa shughuli za uchumi wa buluu ili kubaini uhitaji unaopaswa kutolewa kwa wananchi.

Dkt. Tumaini alisema hata wanapoandaa kozi mpya zinazopaswa kufundishwa, itawapa fursa kutambua uhitaji wa msingi wa watu hao.

# Jinsi DMI ilivyobeba Jukumu la Kuutangaza Uchumi wa Buluu

"Tunashiriki kikamilifu katika kutangaza dhana ya uchumi wa buluu kwa sababu, hata tunapoitwa kutoa ushauri, tunafanya hivyo kupitia kamati za uanzishwaji sera za uchumi wa buluu na maeneo mengine ili kuisaidia serikali," alieleza Dkt. Tumaini.

Hata hivyo, Dkt. Tumaini, aliwataka Watanzania hasa vijana ambao ndilo kundi kubwa kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 kwa Tanzania Bara na Visiwani kuchangamkia fursa zinazotokana na uchumi wa buluu.

Aidha, alitoa wito kwa wazazi na walezi, kuondoa dhana kuwa ubaharia ni uhuni, na kwamba wanapaswa kutambua ni fani kama zilivyo nyingine na kuna fursa nyingi hivi sasa kupitia uchumi wa buluu.

Alizitaja fursa zilizopo sasa kuwa ni ujenzi wa meli kwani kwa sasa DMI inatoa kozi ya Usanifu wa Meli, Uchimbaji wa mafuta na gesi baharini, hivyo vijana wasipochangamka na kuingia katika kada za ubaharia, itatoa mwanya watu kutoka nchi zingine kufanya kazi zinazoweza kufanywa na wazawa.

"Miongoni mwa wanaosoma hapa chuoni niraia wanaotoka nje ya Tanzania, Hivyo ni vyema nafasi katika miradi mbalimbali, zikachukuliwa na Watanzania, siyo raia wengine wa kigeni.

# Ushirikiano wa DMI na Taasisi za Ndani na Nje ya Nchi

Katika kuboresha huduma zake, Chuo kimeendelea kuingia kwenye mashirikiano rasmi na Taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi ikiwemo Chuo cha Taifa cha Utalii Tanzania, Korea Institute of Maritime and Fisheries Technology cha Korea ya Kusini na Italian Shipping Academy cha Genoa Italy na Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA)

## MASHIRIKIANO KATI YA CHUO CHA BAHARI NA CHUO CHA UTALII TANZANIA.

Chuo cha Bahari Dar es Salaam na Chuo cha Taifa cha Utalii tarehe 9 Aprili, 2023 kilifungua fursa mpya ya ajira kwa vijana wa Kitanzania na nje ya nchi, kwa kusaini mkataba wa makubaliano ya kutoa Elimu na Mafunzo ya Ubaharia,




*Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam Dkt.Tumaini Gurumo wa pili kushoto na Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Utalii Dkt.Florian Mtey wa pili kulia, wakisaini mkataba wa makubaliano (MoU).Kushoto na kulia (waliosimama) ni wanasheria wa taasisi hizo*

Wapishi Melini, unaolenga kukuza elimu na kuzalisha wataalamu mahiri watakaokidhi vigezo vya kimataifa katika tasnia ya Bahari na Utalii wa Meli.

Akizungumza wakati wa utiaji saini wa mkataba uliofanyika kwenye ukumbi wa Chuo cha Taifa cha Utalii Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es salaam, Dkt. Tumaini Gurumo alisema kuwa ,Chuo cha Bahari kimebobea katika fani za Ubaharia na kina Ithibati ya kimataifa na Chuo cha Utalii kimebobea kwenye mafunzo ya utalii hivyo muunganiko huo utaleta tija ya uchumi wa buluu.

Aliongeza kuwa, mkataba huo utasaidia juhudi na mikakati ya Serikali kwa kubainisha fursa za ajira ili kuwawezesha vijana wa Kitanzania kuzitumia kwa lengo la kujikwamua kiuchumi kupitia fedha za kigeni, ongezeko la mzunguko wa fedha na hatimaye kukuza uchumi wa Taifa kwa ujumla.

## MASHIRIKIANO KATI YA DMI-NA CHUO CHA UVUVI CHA KOREA YA KUSINI.

Tarehe Septemba 24, 2023 Chuo cha Bahari (DMI)kiliingia makubaliano ya miaka mitano ya kubadilishana uzoefu wa elimu ya Ubaharia na

ujenzi wa Meli na Chuo cha Korea Institute of Maritime and Fisheries Technology ambayo yatawezesha kunufaisha pande zote mbili za vyuo hivyo kwa walimu na wanafunzi .

"Chuo cha Korea Istitute of Maritime and Fisheries Technology (KIMFT) kimeendelea kwa Teknolojia ya Ujenzi wa Meli na Elimu ya Ubaharia na wana vifaa vya kisasa hivyo ni muhimu sana kwa Chuo cha DMI kupata nafasi hiyo muhimu ya kushirikiana na Chuo hicho" Alisema Dkt. Gurumo.

Dkt. Gurumo aliongeza kuwa makubaliano hayo yatawezesha wanafunzi wa Chuo DMI kwenda Chuo cha KIMFT nchini Korea kujifunza elimu kwa Vitendo ili wanafunzi hao waendane na soko la Dunia pamoja na wanafunzi kutoka KIMFT kuja DMI kujifunza kuhusu Elimu inayotolewa.




*Mkuu wa chuo cha Bahari Dar es Salaama (DMI) Dkt Tumaini Gurumo kushoto na Mwakilishi wa chuo cha KIMFT Dkt. Min Jung wakionesha nyaraka za makubaliano mara baada ya kuzisaini.*

## MASHIRIKIANO KATI YA CHUO CHA BAHARI NA CHUO CHA ITALIA

Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) kiliingia makubaliano ya Mashirikiano ( MoU) na Chuo cha Italian Shipping Academy Kilichopo nchini Italia.

Makubaliano haya yalifanyika Nchini Italia Oktoba 19, 2023 kati ya Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam Dkt.Tumaini Gurumo na Rais wa Chuo cha Italian Shipping Academy (FAIMM) Eugenio Massolo kwa lengo la kubadilishana uzoefu katika mafunzo ya ubaharia na kushirikiana katika tafiti na miradi ya maendeleo ya uchumi wa buluu.



*Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam Dkt.Tumaini Gurumo na Rais wa Chuo cha Italian Shipping Academy(FAIMM) Eugenio Massolo wakionesha mikataba yaliyoshuhudiwa na Balozi wa Tanzania Nchini Italia Balozi Mahmoud Thabit Kombo*

Kwa upande wake Mkuu wa chuo cha DMI Dkt. Tumaini Gurumo alisema kuwa makubalino hayo ya Miaka mitano yatasaidia kuongeza ujuzi kati ya Wanafunzi na Wahadhiri kwa pande zote mbili.

"Nimefurahi sana kuingia Makubaliano haya kwa kua wenzetu wapo tayari kushiriana nasi katika miradi mbalimbali, ninaona ndoto ya kufikia viwango vinavyokubalika na EU inakwenda kutimia" Alisema Dkt. Gurumo.

Makubaliano hayo yalishuhudiwa na mabalozi kutoka Tanzania, Balozi Mahmoud Thabit Kombo na Balozi wa Italia nchini Tanzania Balozi Marco Lombardi.

# Ushirikiano wa DMI na Taasisi za ndani na nje ya Nchi

Balozi Mahmoud Thabit Kombo alisema kuwa wenzetu wapo mbele kiteknolojia na Mafunzo na wapo tayari kufanya kazi na DMI, hivyo ni muhimu nasi tuwe tayari na kufanya jitihada kuonyesha ushirikiano ili uhusiano uzae matunda.

### MASHIRIKIANO KATI YA CHUO CHA BAHARI NA MAMLAKA YA UDHIBITI MKONDO WA JUU WA PETROLI (PURA)

Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) kilisaini hati ya makubaliano ya ushirikiano (MOU) na Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA).

Hati iliyosainiwa inahusu mashirikiano ya mafunzo kwenye sekta ya mafuta na gesi ili kuweka msingi katika kuwezesha uanzishwaji wa kituo chenye ithibati kitakachotoa mafunzo ya usalama na kujihami kwa watanzania wanaofanya na wanaotarajia kufanya kazi baharini wakati wa utekelezaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia.

Kwa niaba ya Taasisi wanazo zisimamia Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam Dkt. Tumaini Gurumo na Mkurugenzi Mkuu wa PURA Mhandisi Charles Sangweni walisaini hati hizo za mashirikiano katika hafla iliyofanyika Machi 13, 2024 Jijini Dar es Salaam ambapo menejimenti za pande zote mbili zikiongozwa na Wenyeviti wa Bodi zilishuhudia tukio hilo.

Mkuu wa Chuo alisema, Chuo cha bahari Dar es Salaam kina jukumu la kuandaa rasilimali watu kwa ajili ya sekta zote zinazogusa bahari, mito na maziwa. Hivyo, ushirikiano huu ni wa msingi katika kuwezesha




*Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam Dkt. Tumaini Gurumo na Mkurugenzi Mkuu wa PURA Mhandisi Charles Sangweni wakisaini hati za makubaliano, kushoto na kulia ni wanasheria wa taasisi hizo*

watanzania kupata mafunzo ambayo yatawawezesha kushiriki ipasavyo katika sekta ya gesi na mafuta kwa faida ya jamii na ukuaji wa uchumi wa nchi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) Mhandisi Charles Sangweni alisema kuwa, kuanzishwa kwa kituo cha mafunzo kupitia mashirikiano hayo kutawezesha Watanzania wengi kupata mafunzo stahiki, hivyo kuongeza ushiriki wa wananchi katika shughuli za mafuta na gesi asilia zinazotekelezwa Baharini, kwani kwasasa hapa nchini hakuna kituo chenye ithibati kinachotoa mafunzo ya masuala ya usalama na tahadhari ambayo yanamlazimu kila mfanyakazi wa maeneo ya utafutaji na uchimbaji wa gesi na mafuta kuyapata nje ya nchi.

Aidha, Wenyeviti wa Bodi ya DMI na PURA walipongeza menejimenti na bodi zote kwa kuridhia mashirikiano hayo yanayolenga kukuza ustawi wa jamii na maendeleo ya Taifa kupitia mafuta na gesi asilia vinavyopatikana baharini.



*Picha ya pamoja ya viongozi wa DMI mara baada ya hafla ya kusaini MoU na PURA*

# DMI yapongezwa kwa Kuzalisha Wataalamu Wanaoendana na Ukuaji wa Teknolojia




*Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda akizungumza kuhusu uboreshaji wa huduma ya elimu na mafunzo kwa Mkuu wa Chuo Dkt.Tumaini Gurumo (Kulia) alipotembelea banda la DMI kwenye maonesho ya Wiki ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu.*

Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda alikipongeza Chuo cha Bahari Dar es Salaam kwa elimu na mafunzo inayotoa kwa kuzalisha wataalamu wenye uwezo wa kubuni vifaa vinavyoendana na teknolojia katika sekta ya Elimu.

Pongezi hizo alizitoa Mei 27, 2024 alipotembelea banda la Chuo cha bahari wakati wa ziara ya kupitia mabanda ya washiriki kwenye maaadhimisho ya Wiki ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika Tanga kwenye Viwanja vya Shule ya Sekondari Popatlali kuanzia Mei 25 hadi 31, 2024 kwa lengo la kuibua bunifu na kukuza teknolojia katika sekta ya Elimu.

Chuo cha Bahari Dar es Salaam kilishiriki maonesho haya kwa kuonyesha bunifu mbalimbali, ikiwemo roboti ya kuhamisha mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine, mashine ya kufunga mifuniko ya chupa inayotumika viwandani, udhibiti wa balbu ya mbali, na mfumo wa udhibiti wa joto wa automatiki unaotumika kupoza joto kwenye ghala, pamoja na mfumo wa kugundua uvujaji wa mafuta wa moja kwa moja.




*Mwanafunzi Julius Masaka akitoa ufafanuzi wa utendaji kazi wa Roboti ya kuhamisha mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa mgeni rasmi wa ufunguzi wa maonesho ya wiki ya Elimu Mhe. Prof. Adolf Mkenda alipoambatana na viongozi wengine kwenye ziara ya kutembelea mabanda ya washiriki wa maonesho hayo.*




*Watumishi wa DMI wakitoa huduma kwa wanafunzi waliotembelea banda la DMI kwenye maonesho ya Wiki ya elimu.*

Aidha, Mbali na bunifu hizo Chuo kilishiriki maonesho hayo kwa kutoa huduma za usajili kwa wanafunzi wa mwaka wa masomo 2024/2025, ushauri kwa wanafunzi kuhusu kozi za kusoma kulingana na ufaulu wao, elimu kuhusu matumizi sahihi ya vifaa vya uokozi vinavyotumika kwenye usafiri wa njia ya maji pamoja na kuoa elimu kuhusu fursa zitokanazo na Sekta ya Bahari.

# Baraza la Sita la Wafanyakazi wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam Lazinduliwa



*Mwenyekiti wa Bodi ya Magavana wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) Nahodha Ernest Bupamba akizungumza na Wajumbe wa Baraza la Sita la Wafanyakazi wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam*

Mwenyekiti wa Bodi ya Magavana wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) Nahodha Ernest Bupamba alizindua rasmi Baraza la Sita la Wafanyakazi wa DMI siku ya Ijumaa Machi 22, 2024 kwenye ukumbi wa Mwalimu Nyerere Foundation Jijini Dar es Salaam.

Akizindua Baraza hilo, Nahodha Bupamba aliwapongeza wajumbe wa Baraza kwa maandalizi ya mkutano huo na kusema kuwa ili Taasisi iweze kuendelea ni lazima kushirikisha wafanyakazi wote ili kuwajengea kujiamini na kuwa huru kuchangia mawazo yao kwa maendeleo ya Chuo.

Aidha, Nahodha Bupamba aliwashauri wajumbe wa menejimenti ya Chuo kujenga utaratibu wa kuwapongeza watumishi wanaotekeleza majukumu yao vizuri ili kuleta motisha na kutoa adhabu kwa wale wasiotekeleza majukumu yao kwa kufuata taratibu na kanuni za Utumishi wa Umma.

Naye, Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam Dkt. Tumaini Gurumo aliwashukuru viongozi wa RAAWU kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiutoa kwa Chuo tangu kuzinduliwa kwa Baraza la kwanza na kuwasihi kuendeleza ushirikiano huo.

Aidha, Aliwapongeza watumishi wote wanaojitoa kwa moyo kuwajibika katika kutekeleza majukumu yao kwa maendeleo ya Chuo na Taifa kwa ujumla na kuwasisitiza wengine kuongeza jitihada za utendaji kazi katika maeneo yao.

Akitoa elimu ya ufanyaji kazi wa Baraza kwa Wajumbe, Kamishna wa kazi Bi. Vailet Ndenza alisema kuwa mbali na Baraza kuwa takwa la kisheria pia linasaidia kuimarisha mahusiano mahala pa kazi.

Aliongeza kuwa Baraza huleta amani na utulivu kwa watumishi na kuongeza tija na ufanisi wa huduma inayotolewa na taasisi.



*Picha ya Pamoja baina ya* ***wenyekiti wa Bodi ya Magavana Nahodha Ernest Bupamba (katikati),Mkuu wa Chuo Dkt. Tumaini Gurumo (kushoto) na Kamishna wa kazi Bi. Vailet Ndenza( kulia) na Wajumbe wateule wa Baraza la Wafanyakazi***

# DMI Yatakiwa Kuhamasisha Vijana wa Kike Kujiunga na Fani za Ubaharia.

Waziri wa Uchukuzi Mhe.Prof. Makame M. Mbarawa amekitaka Chuo cha Bahari Dar es Salaam kuongeza jitihada za kuhamasisha Vijana wa kike kujiunga na fani za ubaharia ili kuongeza idadi ya wataalamu wa kike kwenye sekta usafirishaji kwa njia ya maji kama ilivyo kwenye sekta ya anga.

Waziri ameyazungumza hayo leo alipokuwa akifungua maonesho ya wiki ya maadhimisho ya siku ya Bahari duniani, yaliyofanyika Kitaifa Zanzibar-Pemba kwenye viwanja vya Gombani kuanzia tarehe 25 hadi 28 Septemba 2023.



*Waziri wa Uchukuzi Mhe.Prof.Makame M. Mbarawa (wa pili kushoto) katika picha ya pamoja na viongozi wa taasisi mbalimbali baada ya ufunguaji wa maonesho ya maadhimisho ya siku ya Bahari Duniani*

Mhe. Prof. Makame alisema kuwa kumekua na muitikio mdogo sana kwa watoto wa kike kujiunga na fani za masomo ya Ubaharia wakati ni fani zinazosomwa na vijana wa jinsi zote yaani wakike na kiume.

"Fani hizi za Ubahari sidhani kama ni ngumu kama vijana wengi ambavyo hudhani na kuona kama ni fani za wanaume pekee, Ubaharia ni taaluma nzuri, ni wakati sasa kuona namna bora ya kufanya ili kuhamasisha vijana wa kike kujiunga na fani za ubaharia ili kuwainua kiuchumi lakini pia kwa maendeleo ya Taifa kwa Ujumla"Alisema Mhe.Prof. Makame

Aliongeza kuwa , asilimia kubwa ya Uchumi wa Duniani unategemea usafiri wa maji, hivyo ni muhimu kuwa na vijana wa jinsi zote kwenye sekta hii kama ilivyo kwenye anga ili kupanua wigo wa fursa za ajira ndani na nje ya Nchi.



*Mhadhiri Msaidizi Injinia Daniel Rukonu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam akitoa elimu kwa wageni waliotembelea Banda la Chuo Cha Bahari kwenye maonesho ya maadhimisho ya Wiki ya Bahari Duniani*

Tanzania kupitia Sekta zote za Usafiri kwa njia ya maji ziliungana na Dunia kuadhimisha kilele cha siku ya bahari ambayo hufanyika kila Alhamisi ya mwisho wa mwezi wa tisa.

Elimu ilitolewa kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutunza mazingira ya bahari, kuelimisha wanafunzi fursa zitokanazo na masomo ya fani za ubaharia katika kuchagiza Sera ya Uchumi wa Buluu na kurudisha kwa jamii (CSR) kwa vivuko vilivyopo pemba.

Maadhimisho ya siku ya Bahari Duniani kwa mwaka 2023 yalibebwa na kauli mbiu ya "MIAKA 50 YA MARPOL: UWAJIBIKAJI WETU UNAENDELEA".

# Uongozi wa International Maritime Organisation (IMO) Watembelea DMI Kuona Maendeleo ya Utendaji Kazi

Uongozi wa IMO ukiongozwa na Mhandisi Mkuu Milhar Fauzudeen, William Azumo, pamoja na Nahodha Dave Ngui Muli ulifanya ziara katika Chuo cha Bahari Dar es Salaam(DMI) kwa lengo la kuangalia maendeleo ya utendaji kazi wa kitaaluma wa Chuo.

Akizungumza wakati wa kikao kifupi kilichofanyika kwenye ukumbi wa chuo, Mkuu wa Chuo Dkt.Tumaini Gurumo alisema chuo kimepewa mamlaka ya kutoa elimu inayohusiana na mambo ya Bahari katika Ngazi ya Cheti, Astashahada, Stashada na Shahada ya uzamili, hivyo kinahitaji kuongeza miundombinu bora ili kufanya kiweze kutoa mafunzo kwa upana zaidi.





Mhandisi Milhar Fauzudeen alizungumza kuwa Chuo kinatakiwa kiongeze miundombinu ili kuweza kutoa mafunzo kwa ustadi zaidi, na kushauri uongozi wa Chuo kuongeza ushirikiano na Vyuo vya nje vinanvyotoa mafunzo ya Ubaharia ili kujifunza zaidi.

Ofisa William Azumo pamoja na kukipongeza Chuo kwa kufunga mtambo wa kisasa kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi, pia alishauri kuwa ni vyema Chuo kuweka hati (documents) mbalimbali kutoka IMO katika maktaba yake kwa ajili ya rejea(reference) kwa Wanafunzi na Walimu.

Katika kikao kilichofanyika kwenye ukumbi wa chuo waliweza kujadili ajenda mbali mbali ambazo zinalenga kuleta maendeleo katika Chuo cha DMI katika nyanja ya Taaluma na Mafunzo.

IMO ni Taasisi inayosimamia shughuli zote za Bahari duniani ikiwamo mazingira, usalama wa vyombo vya majini na kusimamia Vyuo vinavyotoa mafunzo ya masuala ya Bahari kuhakikisha vimekidhi vigezo stahiki.



*Picha ya pamoja baina ya uongozi wa IMO na wataalam wa Chuo cha Bahari Dar es salaam, walipotembelea chuoni kuangalia mazingira ya utendaji kazi.*

# DMI, TASAC na Mamlaka ya Bahari ya Bahamas Kushirikiana Kukuza Sekta ya Usafiri wa Majini



Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Dkt. Tumaini Shabani Gurumo, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Bw. Kaimu A. Mkeyenge na Naibu Mkurugenzi wa Idara ya Ajira za Mabaharia, Nahodha. Oli Olsen walikutana katika Ofisi za Mamlaka ya Bahari ya Bahamas mjini London, Uingereza  Juni 5, 2023 kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali ya sekta ya usafiri majini.



Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa ni pamoja na kutambuliana vyeti vya mabaharia (Recognition of Seafarers Certificate) na mafunzo kati ya DMI, TASAC na Mamlaka ya Bahari ya Bahamas.

Halikadhalika, walizungumzia suala la Mabaharia wa Kitanzania kupatiwa mafunzo katika meli zilizosajiliwa na Mamlaka ya Bahari ya Bahamas.



*Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Dkt. Tumaini Gurumo,(wa kwanza kushoto) Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Bw. Kaimu A. Mkeyenge (katikati) na Naibu Mkurugenzi wa Idara ya Ajira za Mabaharia, Nahodha. Oli Olsen wakiwa kwenye picha ya pamoja .*

Kwa upande wake Nahodha. Oli kwa niaba ya Mamlaka ya Bahari ya BAahamas aliahidi kushirikiana na Mamlaka zinazosimamia masuala ya Mabaharia nchini yaani DMI na TASAC hususani katika maeneo ya kutambualiana vyeti na mafunzo ili kukuza sekta ya usafiri majini nchini Tanzania.

# Wahitimu 1,326 Watunukiwa Vyeti kwenye Mahafali ya 19 DMI

Jumla ya Wanafunzi 1326 wamehudhurishwa na Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe.David Kihenzile Novemba 30, 2023 kwenye Mahafali ya 19 ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI).

Miongoni mwao wanafunzi 9 ni wa Shahada ya Uzamili, 241 wa Shahada, 192 wa Stashahada , 323 wa Astashahada , 532 wa Astashahada ya Awali pamoja na wanafunzi 29 wa Vyeti vya Umahiri (CoC).

Jumla ya Wanafunzi 1326, Wanafunzi Wakike ni 403 na Wakiume ni 923 .

Chuo Cha Bahari Dar es salaam (DMI)ni kimoja kati ya vyuo vinne (4) vya kikanda barani Afrika; na kinafanyiwa ukaguzi na shirika la kimataifa linalosimamia masuala ya bahari (IMO) kila baada ya miaka mitano ili kuhakikisha ubora na kutambulika kimataifa kwa kozi za ubaharia na kozi za umahiri kwa maafisa wa meli.

Aidha, Chuo kina cheti cha Ubora cha ISO 9001:2015.

Kozi za kitaaluma zinazotolewa na chuo zina ithibati ya NACTVET.

Chuo kinatoa kozi ndefu yaani kuanzia Cheti mpaka kozi za Shahada ya Uzamili, na kozi za muda mfupi yaani (Short Courses) pamoja na kozi za Cheti cha Umahiri (Certificate of Competence).



*Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe.David Kihenzile (wa pili kushoto) akikabidhi vyeti kwa baadhi ya wahitimu kwenye mahafali ya 19 ,wa kwanza kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi Nahodha. Ernest Bupamba, wa tatu kushoto ni Mkuu wa Chuo Dkt,Tumaini Gurumo , anayefuatia ni Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma Dkt.Wilfred Kileo*

Katika kupanua wigo wa fursa za ajira Chuo kimeendelea kufanya utafiti wa uhitaji wa rasilimali watu na kuandaa mitaala mipya na kurekebisha iliyopo ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira katika sekta ya bahari.

Aidha, kupitia kitengo cha ‘DMI Crewing Agency’ DMI imeendelea kushiriki kwa dhati katika kutekeleza adhma ya Serikali yetu ya kuongeza ajira kwa vijana kwa kuwatafutia kazi ndani na nje ya nchi.



***Baadhi ya wahitimu waliosimama wakitunukiwa shahada zao wakati wa sherehe za mahafali ya 19 yaliyofanyika kwenye viwanja vya Chuo (DMI)***

# Serikali Yaombwa Kuipatia DMI Meli ya Mafunzo kwa Vitendo



*Mkurugenzi wa Mamlaka ya Bahari Zanzibar, Bi.Sheikha Mohamed akifungua kongamano la pili la kitaaluma na kutoa rai ya ununuzi wa meli ya mafunzo ili kukiwezesha chuo.*

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Bahari Zanzibar, Bi.Sheikha Mohamed aiomba Serikali kukiwezesha Chuo Cha Bahari Dar es salaam kuwa na Meli ya Mafunzo kutokana sehemu kubwa ya Elimu inayotolewa kuwa ya vitendo zaidi ya nadharia.

Akifungua Kongamano la pili la kitaaluma kwenye viwanja vya DMI Novemba 29, 2023 Mkurugenzi alisema kuwa, Chuo kinazidi kukua, na fani hii ni ya mafunzo kwa vitendo zaidi, hivyo wakati umefika wa Chuo kuwa na Meli yake ili kuzalisha wataalamu watakaoendana na teknolojia katika sekta ya Bahari.

Aliongeza kuwa, katika kufungua fursa za Uchumi wa Buluu mbali na kuwa na Meli ya vitendo pia ni vyema Chuo kujikita katika nyanja zingine katika kufungua fursa na kwamba upo umuhimu kwa Serikali kukitazama Chuo kwa jicho la pili katika kukiwezesha ili fursa zitakazofunguliwa ziweze kuendana na teknolojia.

“ Asilimia kubwa ya wataalamu wanaofanya kazi kwenye sekta hii ya maji ni Wanafunzi kutoka Chuo hiki, na niseme, vijana wapo vizuri na wana weledi, natoa rai kwa Chuo kuhakikisha kinaenda sambamba na fursa hizi kama za utalii, uvuvi, michezo ya baharini na eneo la mafuta na gesi.” Alisema Mkurugenzi.

Naye Mkuu wa Chuo Cha Bahari Dar es salaam Dkt Tumaini Gurumo alisema kuwa Kongamano hilo ni sehemu ya kusherehekea kazi inayofanywa na Chuo yaani ya kutoa Elimu na mafunzo ya Bahari.

Alisema kuwa Kongamano hilo limewakusanya wadau na wanafunzi waliowahi kupata Elimu na Mafunzo chuoni (Alumni) ili kuwasikia ni kwa kiwango gani wamefanikiwa, mitazamo na maoni yao juu ya maendeleo ya Chuo na uboreshaji wa huduma inayotolewa.

Aidha Dkt.Tumaini aliwakaribisha watanzania wote kuja kupata Elimu na mafunzo katika Chuo Cha Bahari kama kauli mbiu inavyosema kufungua fursa za Uchumi wa Buluu, uliolenga ushirikishaji wa watanzania katika kujipatia faida ya kiuchumi kupitia matumizi Bora ya maji yaliyopo kwenye Bahari, Mito na Maziwa.




*Mwenyekiti wa Bodi ya DMI Nahodha. Ernest Bupamba akichangia mada wakati wa majadiliano ya mada zilizowasilishwa kwenye kogamamo la pili la kitaaluma.*

# Wajumbe wa Bodi DMI Waishukuru Serikali kwa Kukiwezesha Chuo Mtambo wa Mafunzo kwa Vitendo



*Wajumbe wa Bodi wakipata maelezo ya utendaji kazi wa mtambo huo kutoka kwa mtaalamu wa mtambo na mkufunzi wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam, Elinathan Blasius(aliyeketi) , walipotembelea kuona mtambo huo.*


Wajumbe wa Bodi ya Chuo cha Bahari Dar es salaam (DMI) walifanya ziara ya kuona utendaji kazi wa mtambo wa kisasa wa kufundishia CRANE SIMULATOR wenye thamani ya Bilioni 2.5 unaolenga kuongeza tija ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa kozi za usafirishaji na lojistiki.

Wajumbe wa Bodi walipongeza hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuwezesha Chuo kupata mtambo huo utakao zalisha wataalamu watakaoendana na teknolojia katika kukidhi soko la ajira.

Mtambo huo utatumika kuzalisha wataalamu watakaofanya kazi maeneo ya Bandari, Viwandani na Migodini.

Mkuu wa Chuo Dkt. Tumaini Gurumo alisema Mtambo huo (Crane Simulator) utasaidia kufundishia wanafunzi kwa vitendo na kuongeza thamani ya elimu inayotolewa katika Chuo hiki pekee hapa nchini.

Pia, Chuo kinakaribisha maombi ya watu binafsi, mashirika na kampuni watakaohitaji kupata huduma ya mafunzo ya namna ya kuendesha mitambo hii ya kisasa ya toleo la Mwaka 2022 kwa ajili ya kuongeza ufanisi mahala pa kazi.



Ziara hii ilifanyika Novemba 11, 2023 katika Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI).



*Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam(DMI) Dkt.Tumaini Gurumo (wa pili kulia) akielezea namna ambavyo Chuo kitanufaika kutokana na kuwepo kwa mtambo huo wa mafunzo kwa vitendo.*

# WOMESA Waendesha Mafunzo Jinsi ya Kufikia Malengo kwa Wanafunzi wa Kike DMI

Umoja wa Wanawake waliopo kwenye Sekta ya Bahari na Bandari (WOMESA) May 19, 2023 waliendesha semina ya mafunzo kwenye ukumbi namba 6 uliopo Chuo cha Bhari Dar es Salaam iliyohusisha wanafunzi wa chuoni kwa lengo la kuwasaidia kufikia malengo yao baada ya kuona changamoto ambazo watoto wa kike wamekuwa wakikutana nazo katika kufikia ndoto zao.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa semina hiyo Makamu Mkuu wa Chuo Fedha, Utawala na Mipango Dkt.Johnson Kileo alisema kuwa, wanawake ni wa muhimu sana katika jamii kwa kuwa Taifa linategemea sana mchango wao katika kuleta maendeleo, na kuongeza kuwa, hakuna mwanaume aliyeweza kusimama bila kuwa na mwanamke hivyo ni muhimu kujiheshimu na kuweka jitihada katika masomo yao pasipo kukata tamaa ili kufikia malengo yao.

Naye Bw. Julius Nguhula aliwasisitiza wanafunzi kuacha tabia za kupenda alama za bure na badala yake waweke jitihada katika masomo yao ili kupata alama halali zitakazowasaidia kuwa bora na kupata utaalamu unaohitajika kwani jamii inahitaji wataalamu wenye weledi na watoto wa kike wanaojitambua katika kuleta maendeleo.



*Baadhi ya wanafunzi wa kike waliohudhuria Mkutano wa WOMESA uliofanyika kwenye ukumbi namba 6 uliopo Chuoni hapo.*

Mshauri wa wanafunzi Chuoni hapo Mhandisi Regina Mbilinyi aliwataka wanafunzi wa kike kuwa na ushirikiano baina yao ili kujenga umoja kati yao na kuwa imara pamoja na kuacha tabia ya kutoa visingizio mbalimbali vinavyopelekea kukosa masomo na mitihani.

Naye mwanasaikolojia Bi. Fides Filbert aliwashauri wanafunzi kutumia ofisi ya mshauri vyema ili kuepuka msongo wa mawazo utakaopelekea kushindwa kufikia ndoto zao.

Semina hiyo inatarajiwa kuwabadilisha wanafunzi wa kike wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam kuwa na mtazamo chanya ambao utawasaidia katika kufikia malengo yao na kuifanya sekta ya bahari kuwa imara.



*Mshauri wa wanafunzi Mhandisi Regina Mbilinyi akizungumza na wanafunzi wa kike wakati wa semina hiyo*




*Mwenyekiti wa umoja wa wanawake walioppo kwenye sekta ya Bahari na Bandari (WOMESA) Mhandisi Fortunata Kakwaya akizungumza na wanafunzi wa kike, kushoto ni Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma Dkt.Wilfred Kileo na kulia ni Mshauri wa wanafunzi ( saikolojia) Bi.Fides Filbert .*

# Ujumbe Kutoka Chuo Kikuu cha Bahari Duniani Watembelea DMI



*Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam Dkt. Tumaini Gurumo akimkabidhi zawadi Makamu wa Rais wa Masuala ya Taaluma kutoka World Maritime University Profesa Dk.Jens-Uwe Schroder-Hinrichs*

Ujumbe kutoka World Maritime University (WMU) ulitembelea Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) kwa lengo la kuona maendeleo ya utendaji kazi wa Chuo, pia kufuatilia maendeleo ya wataaluma waliowahi kusoma katika Chuo hicho akiwemu Mkuu wa Chuo cha Bahari (DMI) Dkt.Tumaini Gurumo.

Akizungumza kwenye ukumbi wa mikutano wa Chuo baada ya kuupokea ugeni huo Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam asema kuwa ujio wa ujumbe huo unaonesha mwanzo mzuri wa kujenga mahusiano ya kitaaluma utakaolenga kuongeza ufanisi wa rasilimali watu wa tasnia ya Bahari.

“Tumefurahi sana kuupokea ugeni huu, tunaona nuru mpya ya kuimarisha mashirikiano na WMU hususani katika kipindi hiki ambacho Chuo kinaendelea kukua kwa kasi” Alisema Dkt.Tumaini

Makamu wa Rais wa Masuala ya Taaluma kutoka World Maritime University Profesa Dk.Jens-Uwe Schroder-Hinrichs akizungumza na menejimenti ya Chuo asema amefurahi kufika na kuona uhalisia wa maendeleo ya Chuo hususani mwamko wa wanafunzi wanaosoma masomo ya ubaharia ukilinganisha na Nchi za Ulaya.

Pia, Profesa Dkt. Anish Hebbar kutoka WMU alisema wamefurahi kufika Chuoni na kukuta kiongozi Mwanamke ambaye aliwahi kuwa mwanafunzi wao kipindi fulani. Kwao imekua ziara yenye tija katika kubadilishana uzoefu.

Wageni hao walipata fursa ya kutembelea miundombinu mbalimbali ya mafunzo kwa vitendo iliyopo Chuoni na kukutana na wahitimu waliowahi kusoma WMU, yaani Alumni ikiwa ni sehemu ya kufuatilia maendeleo yao na kuona namna wanavyotumia taaluma zao.

World Maritime University ni Taasisi iliyopo chini ya International Maritime Organization (IMO) inayojihusisha na kujengea uwezo taasisi za bahari zilizopo katika nchi zinazoendelea.



*Ujumbe kutoka WMU wakipata maelezo mafupi juu ya uendeshaji wa kituo cha mitihani ya lugha ya kiingereza kwa mabaharia (English Marlins Test Centre) kutoka kwa Msimamizi wa Kituo hicho Elinathan Blasius (wa 1 kulia)*

# Ifahamu kwa Undani Maana na Dhana ya Baharia

**Baharia** (Seafarer) ni mtu anayefanya kazi kwenye chombo cha usafiri majini kama vile baharini, kwenye maziwa au mito mfano wa vyombo hivyo ni boti, mashua, jahazi au meli.

Ubaharia ni kazi kama kazi nyingine mbali na inavyochukuliwa na wengi kua ubaharia ni uhuni.

Ubaharia ni kazi ambayo ili uifanye unahitaji uwe umepata mafunzo stahiki yaliyokubalika kimataifa kwa kua na usawa wa ubora kimataifa ndio maana baharia wa nchi yoyote anaweza kufanya kazi nchi yoyote na kwenye meli yoyote duniani.

Kabla ya kufanya kazi kwenye meli baharia lazima awe amepitia mafunzo maalum ambayo yanaitwa kozi za awali (Basic Safety Courses) kwa mujibu wa Shirika la Kimataifa la Bahari (International Maritime Organization) kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati yanatolewa katika Chuo Cha Bahari Dar es Salaam(Dar es Salaam Maritime Institute) ambazo zipo tano :

1. Mbinu za uokoaji melini(Personal Survival Techniques), 2. Usalama wa kibinafsi na wajibu wa kijamii melini (Personal Safety and Social Responsibility), 3. Huduma ya kwanza (Elementary First Aid) 4. Kuzuia na kupambana moto melini (Fire Prevention And Firefighting) pamoja na 5. mafunzo ya usalama melini (Security Awareness Training).

Baharia anaweza kuchanganyika na baharia mwingine wa taifa lingine na waliosoma vyuo tofauti na wakafanya kazi katika meli moja, na isiwepo tofauti ya kiutendaji kwa kua shirika la kimataifa linalosimamia masuala ya bahari duniani (IMO) limeweka viwango vya mafunzo kwa usawa kote duniani kwa baharia ili wasitofautiane kiutendaji.

Mabaharia melini wamegawanyika kulingana na majukumu yao, mfano kuna wale wa idara ya uongozaji meli, hao kuhakikisha meli inatoka sehemu moja na kufika sehemu nyingine.



*Baadhi ya Mabaharia na Wakufunzi wa Chuo cha Bahari Dar es salaam (DMI) wakiwa kwenye picha ya pamoja ndani ya chumba cha mtambo wa mafunzo kwa vitendo.*

Kwa wale wa Idara ya uhandisi wanahakikisha mitambo na mashine zinakua sawa kutoka mwanzo wa safari hadi mwisho.

Pia kuna idara ndogo ya upishi hii inahakikisha maswala yote ya upatikanaji wa chakula na mambo mengine yanayofanana na hayo yanakua sawa mwanzo wa safari hadi mwisho.

**Meli ina idara kuu 3 kulingana na mgawanyo wa majukumu na vitengo.**

A. DECK DEPARTMENT (Waongoza Meli)

B. ENGINE DEPARTMENT (Wahandisi wa Meli)

C. CATERING DEPARTMENT (Huduma za vyakula)

Idara zote hizo watendaji wake huitwa mabaharia wakiongozwa na Nahodha na mhandisi mkuu (Captain and Chief Engineer) na idadi yao melini hutegemea ukubwa wa meli kwa meli ndogo mabaharia nane (8) wanaweza kukidhi shughuli za meli hiyo ila kwa meli kubwa wafanyakazi hufikia hadi 25 mpaka 30 mfano meli kubwa ya mita 300 hadi 400 inayobeba makasha (Container Ship) inaweza kua na idadi hiyo.

## NANI ANAFAA KUWA BAHARIA.

Ubaharia ni fani ya watu wa jinsi zote, yaani vijana wa kike na kiume, ni kazi ambayo inahitaji wataalamu wa jinsi zote kama taaluma zingine

## UHITAJI NA SOKO LA AJIRA

Soko la ajira la mabaharia ni la ndani na nje ya nchi, ni wataalamu wanaohitajika sana kutokana na kukua kwa usafirishaji na uchumi kwa njia ya maji.

Chuo kinatoa rai kwa vijana wakike na kiume kujiunga na kozi zinazotolewa ili kutanua uwanda wa ajira katika fursa hii adhimu na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

## SIFA ZA KUJIUNGA

Mhitimu wa kidato cha nne awe na D nne isipokuwa masomo ya dini, mhitimu wa Kidato cha sita awe na E mbili isipokuwa masomo ya dini kwa ngazi ya Stashahada na D mbili kwa ngazi ya Shahada.

# DMI Yawashukuru Wadau wa Sekta ya Elimu ya Juu kwa Ushiriki Katika Uhuishaji wa Mitaala



*Baadhi ya Wakufunzi wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam na wadau kutoka nje ya Chuo wakijadiliana kuhusu mitaala inayohuishwa na ile iliyotengenezwa ili kutolea maoni.*

Kaimu Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam Dkt. Wilfred J. Kileo aliwashukuru Wadau mbalimbali kwa michango yao waliyoitoa yenye lengo la kuboresha mitaala iliyotengenezwa na inayohuishwa ili iendane na uhalisia wa soko kabla ya kupelekwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa ajili ya ithibati na matumizi.

Akizungumza wakati wa kufunga majadiliano hayo yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Chuo cha Bahari alisema kuwa, mitaala iliyohuishwa inalenga kuzalisha wataalamu ambao wataendana na mahitaji ya soko na wakati kulingana na taaluma watakazosomea.

“Tunawashukuru kwa muda wenu na michango mliyotoa, tunaheshimu sana michango yenu na tunaahidi kufanyia kazi, hii ni hatma ya vijana wetu, Hivyo ni vyema kuhakikisha kwamba tunamuandaa kijana ambaye ataendana na uhalisia kulingana na kile alichosomea” Alisema Dkt.Kileo



*Makamu Mkuu wa Chuo Dkt. Wilfred J. Kileo akitoa shukurani kwa wadau walioshiriki warsha ya uhuishaji mitaala.*

# Wadau Wakutana Kutoa Maoni kuhusu Mpango wa DMI wa Kukabiliana na Majanga

Akiwakaribisha wakati wa ufunguzi wa warsha hiyo uliofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Bahari Dkt.Gurumo alisema kuwa, ni vyema kuandaa miundombinu ya kukabiliana na majanga ili pindi yanapotokea iwe rahisi kuepuka na kukabiliana na madhara.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo Fedha, Utawala na Mipango Dkt.Lucas Mwisila akifunga warsha hiyo amesema kuwa, Chuo kinapenda kuhusisha wadau katika njanja mbalimbali ili kupata maarifa na uzoefu tofauti tofauti na kwamba maoni na mapendekezo yaliyotolewa yatafanyiwa kazi katika kuboresha mpango huo utakao tumika hata kwa vizazi vijavyo.



*Baadhi ya Wadau walioshiriki kwenye kutoa maoni ya kuandaa mipango wa kujikinga na majanga*

Taasisi kutoka maeneo mbalimbali kama TASAC, TCRA, TTCL, SUMA JKT, Uhamiaji, Hazina, Ziamamoto, REDCROSS, EGA, Polisi Ilala, MARINE POLICE na CRDB Bank walishiriki kutoa maoni yao katika kuboresha mpango wa kukabiliana na majanga wa DMI.

# DMI Yazindua Dawati la Kupinga Ukatili wa Kijinsia

Uongozi wa Chuo cha Bahari Dar es salaam (DMI) umeelekezwa kusaidia dawati la kupinga ukatili wa kijinsia kutekeleza majukumu yake na kuwa endelevu kwa kutenga bajeti itakayosaidia kuendesha shughuli za dawati, kujenga uelewa wa pamoja kwa jamii nzima ya DMI na kushirikiana na wadau wengine kama Polisi ili kutekeleza majukumu kwa ufanisi.

Maelekezo hayo yalitolewa na Mkurugenzi Msaidizi (Utawala) wa Wizara ya Uchukuzi Ndg. Hamid Mbegu wakati wa uzinduzi wa Dawati la kupinga ukatili wa kijinsia DMI uliofanyika kwenye ukumbi wa Chuo Septemba 8, 2023.

Mkurugenzi aliipongeza DMI kwa kutekeleza agizo la Serikali la kuunda dawati linaloshughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia kwani madawati hayo ni vyombo muhimu katika kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza katika jamii kama ya Chuo cha Bahari chenye watu wa aina tofauti.

Aliongeza kuwa Menejimenti ya Chuo inao wajibu wa kulea na kuwezesha dawati hilo kuwa endelevu katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo na wao kama Wizara wataendelea kutoa ushirikiano na kusimamia utekelezaji wa sera hiyo ya Kitaifa .

Makamu Mkuu wa Chuo Fedha Utawala na Mipango Dkt. Lucas Mwisila akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Chuo alisema kuwa, Uongozi wa Chuo utatoa kipaumbele katika kuhakikisha dawati hilo linatekeleza majukumu yake ipasavyo




*Mkurugenzi Msaidizi (Utawala) wa Wizara ya Uchukuzi Ndg. Hamid Mbegu (katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya viongoi wa Chuo na wadau wa dawati la jinsia kutoka nje ya Chuo mara baada ya uzinduzi wa Dawati hilo.*

kwani, ukatili wa kijinsia hauathiri sehemu ya kijamii pekee bali hata sehemu ya kiuchumi, hivyo chuo kitajitahidi kuhakikisha jamii yote ya DMI inalindwa dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Mratibu wa Dawati la kijinsia Vyuo Vikuu na Vyuo vya kati Bi.Gift Sowoya kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii ,Jinsia ,Wazee na Watoto amesema kuwa dawati hili linalenga kutekeleza majukumu matatu ambayo ni kuzuia, kupambana na kuitika dhidi ya matukio ya ukatili wa kijinsia hivyo Menejimenti ya chuo isaidie kutatua changamoto zinazowezekana kwa ngazi yao na kwa zile zilizo juu ya uwezo wao kuzifikisha kwenye vyombo husika ili kupata ufumbuzi sahihi.



*Wajumbe wa dawati la jinsia Chuo cha Bahari Dar es salaam wakiwa wamesimama kujitambulisha kwa baadhi ya timu ya Menejimenti ya Chuo wakati wa uzinduzi wa dawati hilo*

# HABARI KATIKA PICHA



*Makamu Mkuu wa Chuo Fedha Utawala na Mipango Dkt.Lucas Mwisila (wa tatu kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa DMI wakati wa mapokezi ya Makombe ya ushindi wa Timu zilizo chini ya Wizara ya Uchukuzi zilizoshinda kwenye michezo ya Mei Mosi mwaka 2023, ikiwa ni sehemu ya utaratibu wa Wizara kufurahia ushindi na kila Taasisi.*




*Mratibu wa michezo ya Wanafunzi Bw. Mansour Likamba akiwapongeza washindi wa mashindano ya Enterclass competition yaliyoandaliwa na Serikali ya Wanafunzi ya DMI -DAMISO yaliyofanyika kwenye viwanja vya Jakaya Youth Park*

# HABARI KATIKA PICHA




*Wanafunzi wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam wakipokea maelekezo ya mafunzo kwa vitendo yanayohusu mbinu binafsi za kujiokoa na kuoa wengine kutoka kwa Mkufunzi na Nahodha Mohamedi Kauli kabla ya kuanza mafunzo hayo.*



*Makamu Mkuu wa Chuo cha Bahari Taaluma Dkt. Wilfred Kileo akizungumza Wanafunzi na baadhi ya Watumishi wa DMI wakati wa semina ya maadhimisho ya siku ya mazingira Duniani iliyofanyika kwenye ukumbi namba*

# Kozi Zitolewazo na Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)

## PROGRAMU ZA CHETI

| PROGRAMU | UFUPISHO | MUDA | ADA |
|---|---|---|---|
| Basic Technician Certificate (NTA Level 4) in Marine Operations | BTCMO | 1 Year | 1,570,000 |
| Basic Technician Certificate (NTA Level 4) in Naval Architecture and Offshore Engineering | BTCNAOE | 1 Year | 1,570,000 |
| Basic Technician Certificate (NTA Level 4) in Oil and Gas Engineering | BTCOGE | 1 Year | 1,570,000 |
| Basic Technician Certificate (NTA Level 4) in Marine Welding and Fabrication | BTCMWF | 1 Year | 1,240,000 |
| Basic Technician Certificate (NTA Level 4) in Shipping and Logistics Management | BTCSLM | 1 Year | 1,240,000 |
| Basic Technician Certificate (NTA Level 4) in Procurement, Logistics and Supply Chain Management | BTCPLSM | 1 Year | 1,240,000 |
| Basic Technician Certificate (NTA Level 4) in Transport and Supply Chain Management | BTCTSM | 1 Year | 1,240,000 |

## PROGRAMU ZA ASTASHAHADA

| PROGRAMU | UFUPISHO | MUDA | ADA |
|---|---|---|---|
| Technician Certificate (NTA Level 5) in Maritime Transport and Nautical Science | TCMTNS | 1 Year | 1,680,000 |
| Technician Certificate (NTA Level 5) in Marine Engineering | TCME | 1 Year | 1,680,000 |
| Technician Certificate (NTA Level 5) in Naval Architecture and Offshore Engineering | TCNAOE | 1 Year | 1,680,000 |
| Technician Certificate (NTA Level 5) in Mechanical and Marine Engineering | TCMME | 1 Year | 1,680,000 |
| Technician Certificate (NTA Level 5) in Oil and Gas Engineering | TCOGE | 1 Year | 1,680,000 |
| Technician Certificate (NTA Level 5) in Marine Welding and Fabrication Engineering | TCMWF | 1 Year | 1,680,000 |
| Technician Certificate (NTA Level 5) in Shipping and Logistics Management | TCSLM | 1 Year | 1,416,000 |
| Technician Certificate (NTA Level 5) in Procurement, Logistics and Supply Chain Management | TCPLSM | 1 Year | 1,416,000 |
| Technician Certificate (NTA Level 5) in Transport and Supply Chain Management | TCTSM | 1 Year | 1,416,000 |

## PROGRAMU ZA SHAHADA YA UZAMILI

| PROGRAMU | UFUPISHO | MUDA | ADA |
|---|---|---|---|
| Master's Degree (NTA Level 9) in Shipping Economics and Logistics | MSEL | 2 Years | 5,895,000 |
| Master's Degree (NTA Level 9) in Transport and Supply Chain Management. | MTSM | 2 Years | 5,895,000 |
| Master's Degree (NTA Level 9) in Marine Engineering Management | MMEM | 2 Years | 5,895,000 |
| Master's Degree (NTA Level 9) in Maritime Law and International Trade | MITML | 2 Years | 5,895,000 |
| Master's Degree (NTA Level 9) in Maritime Transport and Nautical Science | MMTNS | 2 Years | 5,895,000 |

# PROGRAMU ZA SHAHADA

| PROGRAMU | UFUPISHO | MUDA | ADA |
|---|---|---|---|
| Bachelor Degree in Maritime Transport and Nautical Science | DMI01 | 4 Years | 1,746,000 |
| Bachelor Degree in Marine Engineering Technology | DMI02 | 4 Years | 1,790,000 |
| Bachelor Degree in Shipping and Logistics Management | DMI03 | 3 Years | 1,790,000 |
| Bachelor Degree in Naval Architecture and Offshore Engineering | DMI04 | 4 Years | 1,790,000 |
| Bachelor Degree in Procurement, Logistics and Supply Chain Management | DMI05 | 3 Years | 1,790,000 |
| Bachelor Degree in Transport and Supply Chain Management | DMI06 | 3 Years | 1,790,000 |
| Bachelor Degree in Mechanical and Marine Engineering | DMI07 | 4 Years | 1,790,000 |
| Bachelor Degree in Oil and Gas Engineering | DMI08 | 4 Years | 1,790,000 |
| Bachelor Degree in Mechatronics Engineering | DMI09 | 4 Years | 1,790,000 |

# CHETI CHA UMAHIRI

| | | |
|---|---|---|
| Master and Chief Mate | 12 Months | 2,560,000 |
| Master and Chief Mate Between 500GT and 3000GT | 1 Year | 2,219,000 |
| Master and Chief Mate on Ship less than 500GT Engaged on Near Coastal Voyage | 6 Months | 1,284,000 |
| Officer in Charge of a Navigational Watch on Ships of 500GT or More | 1 Year | 2,340,000 |
| Officer in Charge of a Navigational Watch on Ships less than 500GT Engaged on Near Coastal Voyage | 6 Month | 1,075,000 |
| Chief Engineer Officer and Second Engineer Officer | 1 Year | 2,560,000 |
| Chief Engineer Officer and Second Engineer Officer on Ships Between 750 kW and 3000kW | 1 Year | 989,750 |
| Officer in Charge of an Engineering Watch | 1 Year | 2,340,000 |
| Officer in Charge of an Engineering Watch on Ships less than 750kW | 6 Month | 1,075,000 |
| Electro-Technical Officer | 1 Year | 1,966,000 |

# KOZI ZA MUDA MFUPI

| PROGRAMME | MUDA | ADA |
|---|---|---|
| Able Seafarer Deck | 6 Week | 600,000 |
| Able Seafarer Engine | 6 Week | 600,000 |
| Advanced Fire Fighting | 1 Week | 300,000 |
| Basic Training for Oil and Chemical Tanker Cargo Operations | 1 Week | 150,000 |
| Crisis Management and Human Behavior | 1 Week | 150,000 |
| Bridge Resource Management | 1 Week | 200,000 |

## KOZI ZA MUDA MFUPI

| PROGRAMU | MUDA | ADA |
|---|---|---|
| Advanced Training for Oil Tanker/Liquidified Cargo Operation | 1 Week | 350,000 |
| Crowd Management | 1Week | 150,000 |
| Dangerous, Hazardous and Harmful Cargoes | 1 Week | 350,000 |
| Electronic Charts Display and Information System (ECDIS) and Automation | 1 Week | 200,000 |
| Elementary First Aid | 1Week | 150,000 |
| Engine-Room Resource Management | 1 Week | 200,000 |
| Fire Prevention and Fire Fighting | 1 Week | 200,000 |
| GMDSS General Operator (GO) | 3 Week | 350,000 |
| GMDSS Restricted Operator (RO) | 3 Week | 350,000 |
| Medical Care | 1 Week | 280,000 |
| Medical First Aid | 1 Week | 280,000 |
| Passenger Safety, Cargo Safety and Hull Integrity | 1Week | 200,000 |
| Proficiency in Fast Rescue Boat | 1 Week | 300,000 |
| Personal Survival Techniques | 2 Week | 250,000 |
| Personal Safety and Social Responsibilities | 1 Week | 120,000 |
| High Voltage Management Level | 1 Week | 200,000 |
| High Voltage Operational Level | 1 Week | 200,000 |
| Leadership and Managerial Skills | 1 Week | 200,000 |
| Leadership and Team Working Skills | 1 Week | 200,000 |
| Automatic Radar Plotting Aid (ARPA) | 1 Week | 200,000 |
| Passenger Ship Safety Training | 1Week | 150,000 |
| Ship Cook | 4 Weeks | 1,270,000 |
| Hydrogen Sulphide | 1 Week | 150,000 |

